# JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA
# BUNGE LA TANZANIA

## MKUTANO WA TATU

## YATOKANAYO NA KIKAO CHA SABA

**28 APRILI, 2016**

**MKUTANO WA TATU - YATOKANAYO NA KIKAO CHA SABA**

**TAREHE 28 APRILI, 2016**

## I. DUA

Saa 3.00 asubuhi Mhe. Job Y. Ndugai (SPIKA) alisoma Dua na kuliongoza Bunge.

**Makatibu Mezani**

1. Ndg. John Joel
2. Ndg. Ramadhan Abdallah
3. Ndg. Asia Minja
4. Ndg. Joshua Chamwela

## II. MASWALI KWA MHESHIMIWA WAZIRI MKUU

Wabunge wafuatao walimuuliza Mhe. Waziri Mkuu maswali:-

| | | |
|---|---|---|
| 1. Mhe. Rashid Abdallah Shangazi | - | CCM |
| 2. Mhe. Mwita Mwikwabe Waitara | - | CHADEMA |
| 3. Mhe. Zuberi Mohammed Kuchauka | - | CUF |
| 4. Mhe. Seif Khamis Said Gulamali | - | CCM |
| 5. Mhe. Kunti Yusuph Majala | - | CHADEMA |
| 6. Mhe. Abdallah Hamisi Ulega | - | CCM |

Saa 3.35 Bunge lilisitishwa kwa nusu saa ili kupisha matengenezo ya *microphone* ambazo zilikuwa hazisikiki vizuri.

Mhe. Spika alitangaza kwamba Bunge likirudia Maswali ya kawaida hayatakuwepo badala yake mjadala wa Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Ofisi ya Rais (TAMISEMI, Utumishi na Utawala Bora) kwa Mwaka 2016/2017 utaendelea.

Saa 4.00 Asubuhi Bunge lilirudia likiongozwa na Naibu Spika (Mhe. Dkt. Tulia Ackson)

## III. HOJA ZA SERIKALI

Wabunge waliendelea kuchangia Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Ofisi ya Rais (TAMISEMI, Utumishi na Utawala Bora) kwa Mwaka wa Fedha 2016/2017 kama ifuatavyo-

| | | |
|---|---|---|
| 5. Mhe. Josephine Tabitha Chagula | - | CCM |

6. Mhe. Mariam Ditopile Mzuzuri - CCM

**MATANGAZO**

Wageni walioko kwenye gallery zote walitambulishwa Bungeni.

7. Mhe. Catherine Valentine Magige - CCM

**TAARIFA**

Mhe. Ester Nicholas Matiko alimtaka Mhe. Catherine Valentine Magige ataje Vijiji ambavyo sh.50M alizoahidi Mhe. Rais Magufuli zimekwenda. Mhe. Catherine Magige alikataa taarifa hiyo na aliendelea kuchangia.

**Kuhusu utaratibu**

Mhe. Maulid Said Ally Mtulia alitumia Kanuni ya 63(3) kueleza kuwa Mhe. Catherine Valentine Magige amesema uongo kwamba sh.50M alizoahidi zimeshaenda vijijini na kutaka afute kauli yake. Kiti kilitoa mwongozo kwamba kwanza Kanuni au utaratibu wa kuomba kuhusu utaratibu hazikufatwa alipaswa kutumia Kanuni ya 68 ndipo atumie Kanuni ya 63(3). Pili, kwa mujibu wa Kanuni ya 63(4) Mbunge mtoa madai ndiye mwenye wajibu wa kuthibitisha bila shaka.

8. Mhe. Saada Mkuya Salum - CCM
9. Mhe. Mch. Peter Simon Msigwa - CHADEMA

**MWONGOZO**

Mhe. Dkt. Hamisi Kigwangalla aliomba Mwongozo kwa Kanuni ya 68(7) na Kanuni ya 63(1) akimtaka Mhe. Mch. Peter Msigwa afute kauli yake ya kusema kuna baadhi ya Mawaziri hawaiungi Mkono Serikali ya Awamu ya Tano na awataje kwa majina.

Kiti kilitoa mwongozo kwamba kwa Kanuni ya 63(4) na (6) maelezo yatatolewa baadaye.

**TAARIFA**

Mhe. Nape Nnauye alitoa taarifa kwamba Mhe. Mch. Peter Msigwa amesema uongo kwani Bunge halijafunikwa na linarushwa asubuhi na usiku na kwenye magazeti na waandishi wa habari wapo Bungeni.

Mhe. Mch. Peter Msigwa alikataa taarifa hiyo. Kiti pia kilisisitiza Wabunge kuacha tabia ya kuzomea kwani ni kinyume cha utaratibu.

10. Mhe. Tunza Issa Malapo

**Taarifa:**

Mhe. Khatibu Said Haji alimpa taarifa mzungumzaji kwamba aliyemshauri Rais Bunge lisirushwe *live* ni Mhe. Nape Nnauye na mpewa taarifa aliikubali taarifa hiyo.

Mhe. Nape Nnauye alitumia Kanuni ya 68(8) kutoa taarifa kwamba Bunge kutorushwa *live* na TBC ni maamuzi ya Bunge lenyewe katika Bajeti iliyopita kwa kuanzisha Studio ya Bunge na wakati huo yeye hakuwa Mbunge.

| | | | |
|---|---|---|---|
| 11. | Mhe. Abdallah Ally Mtolea | - | CUF |
| 12. | Mhe. Stanslaus Haroon Nyongo | - | CCM |
| 13. | Mhe. Ahmed Mabkhut Shabiby | - | CCM |
| 14. | Mhe. Abdallah Dadi Chikota | - | CCM |
| 15. | Mhe. Mwanne Ismael Mchemba | - | CCM |
| 16. | Mhe. Vedastus Mathayo Manyinyi | - | CCM |
| 17. | Mhe. Elias John Kwandikwa | - | CCM |
| 18. | Mhe. Shally Joseph Raymond | - | CCM |
| 19. | Mhe. Godbless Jonathan Lema | - | CHADEMA |
| 20. | Mhe. Frank George Mwakajoka | - | CHADEMA |

## IV. MATANGAZO

- Maswali ya kawaida yaliyobaki yatapangiwa muda na wahusika watajulishwa.
- Wanamichezo walioenda Zanzibar wamerudi ambapo timu ya Netball imeshinda.
- Miongozo na utaratibu iliyoombwa itatolewa majibu baadaye.
- Mhe. Naibu Spika alitoa Mwongozo kwa Mhe. Godbless Lema kuacha kutoa taarifa za uwongo na kuwagombanisha Viongozi wa Bunge kwani urudishaji wa Fedha za Bunge Viongozi walishirikishwa kinyume na alivyoeleza.

## V. KUSITISHA SHUGHULI ZA BUNGE

Shughuli za Bunge zilisitishwa saa 7:00 hadi saa 10:00 jioni.

## VI. BUNGE KURUDIA

Saa:10:00 jioni Bunge lilirejea na kuongozwa na Mwenyekiti wa Bunge Mhe. Najma Murtaza Giga. Uchangiaji uliendelea kwa wafuatao:-

| | | | |
|---|---|---|---|
| 21. | Mhe. Maulid Abdallah Mtulia | - | CUF |
| 22. | Mhe. Ruyagwa Kabwe Zitto | - | ACT |
| 23. | Mhe. Charles John Tizeba | - | CCM |

| | | | |
|---|---|---|---|
| 24. | Mhe. Abdallah Omary Shangazi | - | CCM |
| 25. | Mhe. Jasson Samson Rweikiza | - | CCM |
| 26. | Mhe. George Malima Lubeleje | - | CCM |
| 27. | Mhe. Atashasta Justus Nditiye | - | CCM |
| 28. | Mhe. Augustino Philip Mulugo | - | CCM |
| 29. | Mhe. Richard Philip Mbogo | - | CCM |
| 30. | Mhe. Joseph Osmund Mbilinyi | - | CHADEMA |

**TAARIFA**

Mhe. Hawa Abdulrahman Ghasia alimpa taarifa Mhe. Joseph Mbilinyi kwamba masuala ya Bandari na *Single Custom Territory* yapo nje ya mada inayoongelewa lakini Mhe. Joseph Mbilinyi alikataa taarifa hiyo na aliendelea kuchangia.

| | | | |
|---|---|---|---|
| 31. | Mhe. Lucy Simon Magereli | - | CHADEMA |
| 32. | MHE. Masoud Abdallah Salim | - | CUF |

**Kuhusu utaratibu**

Mhe. Dkt. Hamisi Kigwangala alitumia Kanuni ya 63(1)-(4) akitaka mchangiaji athibitishe kwamba Mhe. Nape Nnauye alitoa taarifa za uwongo Bungeni. Mwenyekiti alieleza kuwa mwongozo utatolewa baadaye na Mhe. Masoud aliendelea kuchangia.

| | | | |
|---|---|---|---|
| 33. | Mhe. Amina Makilagi | - | CCM |

**Taarifa**

Mhe. Hawa Mchafu alitoa taarifa kwa Mhe. Amina Makilagi kwamba uchaguzi wa Serikali za Mitaa Arusha CCM imeshinda na kwamba alichoongea ni kweli kwamba kama uchaguzi ungerudiwa CCM ingeshinda kwa asilimia kubwa. Mhe. Makilagi alikubali taarifa hiyo na aliendelea kuchangia.

| | | | |
|---|---|---|---|
| 34. | Mhe. Oran Manase Njeza | - | CCM |
| 35. | Mhe. Lolesia Jeremiah Bukwimba | - | CCM |
| 36. | Mhe. Jitu Vrajlar Soni | - | CCM |
| 37. | Mhe. Sophia Hebron Mwakagenda | - | CHADEMA |
| 38. | Mhe. Peter Ambrose Lijualikali | - | CHADEMA |

**Taarifa**

Mheshimiwa Jenista Mhagama aliomba mwongozo kwamba Mbunge anayezungumza anatumia Lugha ya maudhi dhidi ya jina la Rais na

Waziri Mkuu na kwamba Rais au Waziri Mkuu hawahusiki na mambo ya uchaguzi na hivyo afute kauli hizo. Mhe. Peter Lijualikali alikubali kufuta Lugha ya maudhi lakini alisisitiza ukweli unabaki kwamba ana Hoja ya Msingi.

39. Mhe. Riziki Shahari Mngwali - CUF
40. Mhe. Mussa Rashid Ntimizi - CCM

Mhe. James Kinyasi Millya alimpa taarifa mzungumzaji kwamba alishinda kwa kutumia jina la Tatu Ntimizi na Mhe. Mussa Ntimizi alikataa taarifa hiyo na kwamba alishinda kwa kura nyingi tu.

41. Mhe. Anna Richard Lupembe - CCM

Mhe Dtk Suleiman Ally Yussuf alitumia Kanuni ya 68(8) na 63 kusema Mbunge anayezungumza anasema uongo kwamba Zanzibar kuna amani wakati siyo kweli kwani Askari wamesambaa kila mahali na wananchi wanateseka. Mhe. Anna Lupembe alikataa taarifa hiyo na kusisitiza Zanzibar kuna amani.

42. Mhe. Lucia Michael Mlowe

**Taarifa**
Mheshimiwa Jacquilline Ngonyani Msongozi alitoa taarifa kwamba Mbunge anayechangia anapoteza muda kwa vile inaonekana hajajipanga na ni bora kuchangia kwa maandishi Mhe. Lucia Mlowe alikataa taarifa hiyo.

43. Mhe. Neema William Mgaya - CCM

**VII. KUAHIRISHA SHUGHULI ZA BUNGE**

Saa 2:00 Usiku Mwenyekiti aliahirisha Bunge hadi siku ya Ijumaa tarehe 29/4/2016 saa 3.00 asubuhi.

**DODOMA** **DKT. T. D. KASHILILAH**
**28 APRILI, 2015** **KATIBU WA BUNGE**